

CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE



MAHAFALI YA KUMI NA SABA (17) KAMPASI YA KIVUKONI NA MAHAFALI YA SABA (7) KAMPASI YA KARUME ZANZIBAR- 2022

Mkuu wa Chuo anawatangazia wanafunzi waliohitimu masomo yao katika mwaka wa masomo 2021/2022 kwamba **Mahafali ya Kumi na Saba** yatafanyika kwenye Kampasi ya Kivukoni, siku ya **Ijumaa tarehe 25 Novemba, 2022** kuanzia saa **TATU ASUBUHI (03:00)** na **Mahafali ya Saba** katika Kampasi ya Karume Zanzibar yatafanyika **Jumatatu tarehe 28 Novemba, 2022** kuanzia saa **TATU ASUBUHI**.

Wahitimu wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1. Kuchukua Majoho kwenye ofisi namba 115 – Jengo la Uhuru **Kampasi ya Kivukoni** kuanzia **Jumatatu, tarehe 21** hadi **Alhamisi, tarehe 25 Novemba, 2022** wakati wa saa za kazi na kwa **Kampasi ya Karume - Zanzibar** wafike Ofisi ya PMU kuanzia **Ijumaa tarehe 25** hadi **Jumapili tarehe 27 Novemba, 2022** kuanzia saa **4:00** asubuhi hadi saa **9:00** alasiri. Majoho hayatatolewa siku ya mahafali.
2. **MALIPO YA MAJOHO NI SHILINGI AROBAINI ELFU NA MALIPO YOTE YAFANYIKE KWA KUTUMIA CONTROL NAMBA.**
3. Majoho sharti yarejeshwe Chuoni kabla ya **tarehe 3 Desemba, 2022** kwa **Kampasi ya Kivukoni na Kampasi ya Karume- Zanzibar**. Vinginevyo faini ya shilingi **10,000/=** itatozwa kwa siku kwa yeyote atakayechelewa kurudisha joho hilo.
4. Zoezi la namna ya kupokea vyeti (**rehearsal**) litafanyika **Alhamis, tarehe 24 Novemba, 2022** kuanzia saa **6.00 mchana** katika uwanja wa Mahafali **Kampasi ya Kivukoni** na kwa **Kampasi ya Karume-Zanzibar** zoezi hilo litafanyika **Jumapili tarehe 27 Novemba, 2021** kuanzia saa **4:00 asubuhi** katika uwanja wa mahafali. **Mhitimu atakayeshindwa kuhudhuria zoezi hilo, hataruhusiwa kushiriki katika Mahafali hayo.**
5. Kila Mhitimu atapaswa kujigharamia usafiri, malazi na chakula.
6. Kusanyiko la wahitimu wote (**CONVOCATION**) waliosoma katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere litafanyika **Alhamis, tarehe 24 Novemba 2022** katika Ukumbi mpya wa Mihadhara (**NEW LT**) chuoni hapo kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa sita mchana.
7. Washiriki wote wa Mahafali wanatakiwa kuthibitisha ushiriki wao katika Ofisi ya Mitihani kabla ya **tarehe 25 Novemba, kwa kupiga simu namba 0782405552 AU 0767245451**

Nyote Mnakaribishwa.

Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere,
S.L.P. 9193,

DAR ES SALAAM.

Simu: +255 22 2820041/ 2820045/ 2820047

Faksi: +255 22 2820816

Barua pepe: rector@mnma.ac.tz